

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA UJENZI**

Simu:+255 26 2324455  
FAX: +255 26 2323233  
Barua pepe: ps@mow.go.tz  
Tovuti: [www.mow.go.tz](http://www.mow.go.tz)



Mji wa Serikali Mtumba,  
S.L.P. 2888,  
**40470 DODOMA.**  
TANZANIA

**DODOMA, 18 Aprili 2024**

**TAARIFA KWA UMMA**

Kufuatia tukio la kuanguka Jengo la Ghorofa mbili katika eneo la Magogoni , jijini Dar es Salaam, Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa (Mb), amezielekeza Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB) na Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiraji Majenzi (AQRB) kufika mara moja eneo la tukio na kushirikiana na timu za Wataalam kutoka Mamlaka nyingine za Serikali kupata sababu ya kuanguka jengo hilo na kuchukua hatua stahiki kwa wale wote ambao wamekiuka Sheria za kitaaluma katika ujenzi na usimamizi wa jengo hilo.

Aidha, amezitaka Bodi hizo kuhakikisha wanaendelea kusimamia miradi ya ujenzi ikiwemo barabara, madaraja na majengo na kuhakikisha wajenzi na wasimamizi wa miradi hiyo wanafanya kazi kwa kuzingatia miiko na maadili ya taaluma zao.

Waziri Bashungwa anatoa pole kwa majeruhi na familia iliyopoteza mpendwa wao na anatoa wito kwa Wakandarasi, Wahandisi na wamiliki wa majengo kuhakikisha wanatumia wataalam waliosajiliwa na Bodi za CRB, ERB na AQRB ili kuepusha kutokea kwa madhara yanayoweza kusababisha majeruhi na vifo, na hivyo kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Imetolewa na;  
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,  
Wizara ya Ujenzi